# DAWASA YETU

TOLEO NO: 203 | TAREHE: 2.6.2025 HADI 8.6.2025

# MWENGE WA UHURU KITAIFA 2025 WATEMBELEA MIRADI YA MAJISAFI YA BILIONI 38.1 DAR.



Mwenge wa Uhuru Kitaifa umehitimishwa katika miradi ya majisafi Dar es Salaam iliyotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (**DAWASA**) huku ukiacha ujumbe kwa wananchi kuwa walinzi wazuri wa miundombinu ya maji pamoja kuwasihii kujitokeza kwa wingi kuunganishiwa huduma kupitia miradi ya majisafi iliyokamilika ili wanufaike na uwekezaji uliofanywa na Serikali ya **Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.**

Mwenge wa Uhuru ulioanza kutembelea miradi ya majisafi mnano tarehe **02.06.2025**, umefanikiwa kutembelea miradi minne, ukiwemo mradi wa maji Kigogo uliopo Kata ya **Kisarawe II** uliotekelezwa kwa **Shilingi 780** katika **Wilaya ya Kigamboni**, mradi wa maji **Mbopo** uliogharimu **Shilingi Milioni 280** uliopo **Kata ya Mabwepande**, **Wilaya ya Kinondoni**, mradi wa maji **Bangulo** uliogharimu **bilioni 36.9**, pamoja na **mradi wa ujenzi wa kituo cha kusukuma maji cha Kibamba**.

Akizungumza wakati akihitimisha Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Kiongozi wa Mbio za Mwenge **Ndugu Ismail Ali Ussi** amesema kuwa miradi hii ya majisafi katika **Jiji la Dar es Salaam** imeleta tija kubwa kwa wananchi kwa **kuwaondolea changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi pamoja na kuongeza usalama wa afya za watumiaji wa maji**.

"Ameipongeza Serikali ya **Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu** Hassan kwa jitihada kubwa za kuwekeza fedha nyingi katika miradi ya majisafi yenye kuleta furaha kubwa kwa wananchi wote wa **Dar es Salaam**," amesema **Ndugu Ussi**.

Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa **DAWASA** Mhandisi Mkama Bwire amemshukuru **Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan** kwa kuipa nguvu **DAWASA** katika kutekeleza miradi mingi ya majisafi yenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa maji kwa wananchi wote wa **Dar es Salaam** ili **kutimiza adhma ya kumtua Mama ndoo kichwani**.

Amewataka wananchi waendelee kujitokeza kwa wingi ili kuunganishwa katika huduma ya majisafi na waweze kunufaika na uwekezaji wa Serikali.

Mmoja wa wanufaika wa miradi ya majisafi **Bi Zuena Mrema** ametoa pongezi nyingi kwa Serikali kwa kuwaletea maji katika makazi yao.

"Jitihada hizi za kuleta miradi ya maji zimekuwa na manufaa kwetu maana tulipata tabu ya maji kwa muda mrefu," amesema.